



# Habari juu ya Virusi vya Corona (COVID-19) na shule – habari kwa wazazi na wanafunzi

Serikali zote za Australia – shirikisho, jimbo na wilaya – zinatambua umuhimu wa elimu na zinaahidi kusaidia kujifunza kwa wanafunzi wakati wa janga la COVID-19.

Serikali za jimbo na za wilaya pamoja na mamlaka ya sekta yasiyo serikali zina jukumu kwa kusimamia na kuamua maamuzi ya uendeshaji kwa shule zao. Kwa habari kuhusu jinsi ya shule katika eneo lako zinavyojibu kwa COVID-19 tafadhali wasiliana na shule yako kwanza, na fuata ushauri kutoka serikali za jimbo au wilaya. Maunganisho kwa tovuti za elimu za serikali za jimbo na wilaya yapo chini:

[Australian Capital Territory](#)  
[New South Wales](#)  
[Northern Territory](#)  
[Queensland](#)  
[South Australia](#)  
[Tasmania](#)  
[Victoria](#)  
[Western Australia](#)

Serikali za jimbo na wilaya zimekubali kuwa maamuzi kuhusu jinsi ya kuvyojibu kwa COVID-19 katika shule yanapaswa kuendelea kujulishwa na ushauri rasmi wa mtalamu wa elimu na afya ya umma waliotegemeza kitaifa na jimbo.

## Kupunguza hatari inayowezekana ya maambukizi ya COVID-19 shuleni

Kwa tarehe ya **24 Aprili 2020**, Kamati Kuu ya Ulinzi wa Afya ya Australia (AHPPC) ilitolea [ushauri wa kiafya\(health advice\)](#) kuhusu kupunguza hatari inayowezekana ya maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19 katika shuleni. Mwongozo wa vitendo na ushauri huu umetayarishwa kwa viongozi wa shule ambao wanashughulikisha na watoto, wazazi, waalimu na wafanyakazi wa msaada ili kupunguza hatari ndogo kiasi hata zaidi ya maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) katika shule wakati wa janga la COVID-19.

Kwa kifupi mambo ya kuzingatia ni pamoja na:

- **Kwa wazazi:** ikiwa mtoto wako ni mgonjwa, anapaswa asiende shule. Unapaswa kumbakisha mtoto nyumbani na mbali na wengine. Kumbuka kudumisha umbali wa mwili kutoka wazazi wengine na waalimu wakati wa kwenda shuleni, pamoja na wakati wa kuacha na kuchukua watoto wako.
- **Kwa watoto:** umwambie mzazi wako, mlezi au mwalimu wako ikiwa ni mgonjwa.

- **Kwa waalimu:** usije kazini ikiwa wewe ni mgonjwa au yupo katika hali ya hatarini.
- **Kwa watu wazima wote:** hatari kubwa ya maambukizi katika mazingira ya shule ni kati ya watu wazima. Ni jambo la muhimu sana kwamba wote waalimu na wazazi wadumishe umbali wa mwili kati yao na kila mmoja shuleni.

## Usafi

Wanafunzi wanakumbushwa:

- Osha mikono yako mara nyingi na sabuni na maji ikiwa ni pamoja na kabla na baada ya kula na baada ya kwenda choo.
- Tumia sanitaiza ya mkono.
- Funika kikohozi chako na kupiga chafya kwa mwiko wako au tishu (sio mikono yako).
- Weka tishu zako zilizotumiwa kwenye pipa mara moja kisha osha mikono yako.
- Jaribu kuacha kugusa mdomo wako au uso wako.
- Usishike mikono, au kushikana mikono na wengine.
- Jaribu kuweka nafasi zaidi kuliko kawaida kati ya kwako na wengine.
- Epuka kusimama kwenye foleni.
- Uombe msaada kutoka wengine ikiwa unajihisi wasiwasi.

## Mipangilio ya sekondari kubwa na viingilio cha chuo kikuu

Kwa tarehe ya 7 Aprili 2020, Waziri wa Elimu wa jimbo pamoja na wilaya walikubaliana kuwa wanafunzi wakubwa wa sekondari (wanafunzi wa mwaka 12) wataweza kupata Cheti cha Elimu cha Sekondari Kubwa mwaka huu, na cheti hiki kitawezesha ufikiaji wa chuo kikuu, elimu zaidi na ajira.

## NAPLAN

Kwa tarehe ya Machi 20, 2020, Waziri wa Elimu waliamua kwamba NAPLAN haitaendelea mnamo 2020. NAPLAN ilipangwa kufanyika tarehe za 12 Mei hadi 22 Mei 2020.

Uamuzi wa kutoendelea na NAPLAN mnamo 2020 umeamuliwa ili kusaidia viongozi wa shule, walimu na wafanyakazi wasaidizi kuzingatia ustawi wa wanafunzi na mwendeleo wa masomo.

NAPLAN ni tathmini ya kitaifa ambayo inapima uwezo wa wanafunzi katika maeneo matatu ya uwezo wa kusoma na kuandika - kusoma, kuandika na mikusanyiko ya lugha (tahajia herufi, sarufi na matamshi) - na uwezo wa hesabu. Shule katika majimbo yote na wilaya zimesimamia NAPLAN mwezi wa Mei kila mwaka tangu 2008.